# Kukabiliana na COVID-19

Tembelea ukurasa huu mara kwa mara kwa taarifa na utembelee coronavirus.wa.gov kwa habari mpya kutoka kwa mashirika kutoka kote katika jimbo kwa lugha za (Kihispania, Kirusi, Kivietinamu, Kichina, Kijapani, Kikorea, Kipunjabi, Kisomali, Kiukreni).

## Jengo la UTC Limefungwa kwa Umma

Jengo la UTC limefungwa kwa umma hadi taarifa zaidi itakapotolewa na wafanyakazi wote wa UTC wanafanya kazi kutoka nyumbani.

Huduma nyingi zinapatikana kwenye tovuti yetu, na unaweza kupiga simu kwa ajili ya usaidizi au kuwasilisha lalamiko la mtumiaji kupitia 1-888-333-WUTC (9882) au upige gumzo mtandaoni kuanzia 8 asubuhi - 5 jioni, Jumatatu-Ijumaa. Huduma za utafsiri kupitia simu zinapatikana.

## Stay Home, Stay Healthy

Mnamo Machi 23, Gavana Jay Inslee alitoa amri ya Stay at Home, Stay Healthy, na mnamo Mei 1 akaongeza muda wa amri na akaanzisha muundo wa awamu nne wa Safe Start Washington wa kurudi katika hali ya kawaida. Kaunti zinapitia awamu hizi kivyake, kwa hivyo kampuni zinahitajika kujua ni mwongozo upi unaotumika kwa kaunti ambapo zinafanya kazi.

- Ili kufafanua hali ya biashara yako au kutuma ombi ili biashara yako ichukuliwe kuwa ya muhimu, tafadhali wasilisha fomu hii (Kiingereza pekee).

## Msaada wa Bili za Huduma

Gavana Inslee alitoa amri ya kupiga marufuku huduma zote za nishati, simu za nyaya, na kampuni za maji kutokana na kukata huduma au kutoza ada ya kuchelewa hadi Julai 28.

- Kampuni zinaweza kupata fedha ili kuwasaidia wateja kulipa bili za huduma.
- Iwapo unahitaji usaidizi katika kulipa bili yako ya huduma, unapaswa kuwasiliana na kampuni yako au uwasiliane na tume kupitia 1-888-333-WUTC (9882) kuanzia saa 8 asubuhi - 5 jioni, Jumatatu-Ijumaa au utume barua pepe kupitia consumer@utc.wa.gov wakati wowote.
- Bado utahitajika kulipa bili zako mara muda wa amri utakapokwisha, kwa hivyo ikiwa unaweza kulipa sasa, basi fanya hivyo.

## Kampuni Zinazodhibitiwa

Tunashirikiana moja kwa moja na kampuni zinazodhibitiwa na UTC za huduma na usafirishaji wakati zinaporekebisha sera na desturi zake wakati huu.

## Maelezo kuhusu kampuni za usafirishaji

### Pipeline and Hazardous Materials Safety Administration (PHMSA)

PHMSA imeruhusu kwa muda mabadiliko katika kutimiza masharti ya mhudumu (Kiingereza pekee) kutokana na kuwa na wafanyakazi wachache na rasilimali duni.

- Mabadiliko katika mahitaji ya upimaji wa dawa,
- Utekelezaji uliosimamishwa wa masharti ya mhudumu na mahitaji ya usimamizi wa chumba cha udhibiti kama vile saa za huduma na mahitaji ya mafunzo maalum.

### Federal Railroad Association (FRA)

- FRA ilitoa salimisho la dharura kwamba, ikiwa kuna uhaba wa mahali pa kazi, itaacha kutekeleza baadhi ya mahitaji ya usalama (Kiingereza pekee).
- UTC itafuata salimisho hili wakati wa kutumia mamlaka iliyopewa ya utekelezaji.

### Wahamishaji wa bidhaa za nyumbani

- Wahamishaji wa bidhaa za nyumbani lazima wavae barakoa za kufunika uso.
- Kwa kaunti zilizo katika Awamu ya Kwanza, wahamishaji wanaweza kufanya tu uhamishaji wa bidhaa kwa mali isiyohamishika ambayo imeshanunuliwa, au mtu aliye katika mazingira hatari ambaye anaondoka mazingira yasiyo salama.
- Kwa kaunti zilizo katika Awamu ya Pili, wahamishaji wanaweza kuanza shughuli zote, iwapo wanaweza kukidhi mahitaji ya usalama ya mwajiri kutoka Department of Labor & Industries.

### Federal Motor Carrier Safety Administration (FMSCA)

- FMSCA iliidhinisha salimisho la muda la mahitaji ya saa za huduma kwa magari ya Biashara yanayowasilisha misaada ya dharura (kama vile vyakula, vifaa vya matibabu, na vifaa vya kinga vya kibinafsi), almradi madereva wanapata saa ya kupumzika baada ya kukamilisha uwasilishaji.
- FMSCA ilichapisha orodha ya maswali yanayoulizwa sana kuhusu taarifa hii kwenye tovuti yake (Kiingereza pekee).
- FMCSA imeunda ukurasa wa maelezo kuhusu Virusi vya Korona (COVID-19) (Kiingereza pekee).

### Department of Licensing (DOL)

- Department of Licensing imeongeza muda tarehe za kumalizika kwa uhalali wa leseni ya udereva kwa siku 30.
- Chini ya miongozo ya FMSCA, DOL inaongeza tarehe za kumalizika kwa uhalali wa leseni za dereva wa kibiashara (CDL) na vibali vya dereva wa kibiashara (CDP) ambazo zimalizika mnamo au baada ya Machi 30 hadi Septemba 30.
- Madereva wa kibiashara wanapaswa kubeba nakala ya cheti chao cha matibabu kilichoishiwa na muda ili kuonyesha kuwa tarehe ya kumalizika kwa uhalali wa leseni au kibali chao ilikuwa mnamo au baada ya Machi 30.

# Mikutano, Usikizaji wa Kesi na Warsha za Hadhara

Tunafanya mikutano, usikilizaji wa kesi na warsha zote za hadhara kupitia simu au mtandaoni. Ikiwa unapanga kushiriki katika tukio la tume, hakikisha umeangalia kalenda kwa maelezo.

## Nyenzo

- Tovuti rasmi ya Jimbo la Washington kuhusu COVID-19 (Kihispania, Kirusi, Kivietinamu, Kichina, Kijapani, Kikorea, Kituruki, Kisomali, Kiukreni).
- Tovuti ya Idara ya Afya (Department of Health) kuhusu Mkurupuko wa Virusi vipya vya Korona 2019 (Lugha ya Ishara ya Marekani (ASL), Kichina, Kijapani, Kikorea, Kituruki, Kirusi, Kisomali, Kihispania, Kiukreni, Kivietinamu).
- Pigia simu ya dharura ya COVID-19 kupitia 1-800-525-0127 iwapo una maswali kuhusu kile kinachotokea katika Washington, au jinsi virusi vinavyoenea. Simu zinafunguliwa kuanzia saa 6 asubuhi hadi 10 usiku, kila siku.
- Ili kuona miongozo ambayo tume za huduma katika majimbo mengine zimetoa, tembelea kifuatilia cha majibu ya jimbo cha NARUC (Kiingereza pekee).

## Ufikiaji

Je, ungependa maelezo haya katika muundo tofauti? Piga simu 1-800-833-6384 au piga 711 kwa Vifaa vya Kupiga Chapa kwa Ujumbe (Text Teletype) (TTY) kupitia Huduma za Muunganisho za Washington (Washington Relay Services).

UTC inaweza kukusaidia katika lugha nyingi. Tafadhali piga simu 1-888-333-9882 kuanzia saa 8 asubuhi - 5 jioni Jumatatu-Ijumaa na uombe kuwa na mkalimani.